**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**689** **VITENDO VYA KUJIFUNZA SAYANSI**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2005**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **40** na sehemu **B** na **C** zina alama 30 kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. (a) Eleza maana ya "makazi salama" kwa mtoto wa elimu ya awali.

   (b) Taja sifa tatu (3) za maji safi na salama ya kunywa.

2. (a) Bainisha njia nne (4) za kuhifadhi chakula kwa usalama nyumbani.

   (b) Eleza kwa kifupi umuhimu wa upumuaji katika mwili wa binadamu.

3. (a) Orodhesha vifaa vinne (4) vinavyopatikana katika kikasha cha huduma ya kwanza.

   (b) Taja vitu viwili (2) ambavyo vinaweza kusababisha majeraha ya moto (kuungua) nyumbani.

4. (a) Nini maana ya neno "ajali"?

   (b) Orodhesha aina tatu (3) za uchafu wa mazingira.

5. (a) Fafanua hatua mbili (2) za kuokoa mtu anayezama majini.

6. Ainisha shughuli nne (4) za vitendo zinazoweza kutumiwa kufundisha wanafunzi wa elimu ya awali kuhusu umuhimu wa kunawa mikono.

7. (a) Taja kanuni mbili (2) za kuzuia moto shuleni.

   (b) Eleza athari tatu (3) za kutumia vyombo vichafu wakati wa kula au kunywa.

8. (a) Bainisha sifa nne (4) za kiwanja bora cha michezo shuleni.

   (b) Eleza kwa kifupi sababu mbili (2) za kutupa taka mahali panapofaa.

9. (a) Orodhesha misismi minne (4) ya kuzingatia unapoandaa **mazingira ya kujifunzia** darasani.

10. (a) Eleza kwa kifupi sababu mbili (2) za michezo ya watoto ya kukimbia na kuruka.

    (b) Taja mambo manne (4) yanayofanywa na mwalimu kumfanya mtoto apende shule.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

11. (a) Jadili faida tano (5) za kutumia maji safi na salama katika maisha ya kila siku.

    (b) Fafanua njia tano (5) zinazoweza kutumiwa kuzuia ajali za watoto katika mazingira ya shule ya elimu ya awali.

12. (a) Eleza madhara manne (4) yanayoweza kumpata mtoto kutokana na kuishi katika makazi yasiyo safi.

    (b) Bainisha faida tatu (3) za elimu ya kazi kwa mwalimu anayefundisha somo la Vitendo vya Kujifunza Sayansi.

    (c) Jadili mambo manne (4) ya msingi ya kuzingatia unapo mfanyia uchunguzi mtoto aliyepata ajali kabla ya kumpa huduma ya kwanza.

13. (a) Kwa nini ni muhimu kwa mwalimu wa elimu ya awali kuwa na ujuzi wa huduma ya kwanza? Toa sababu nne (4).

    (b) Fafanua changamoto tano (5) zinazowakabili walimu katika kufundisha somo la Vitendo vya Kujifunza Sayansi kwa vitendo.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

14. (a) Jadili namna mwalimu atakavyofundisha wanafunzi kuhusu vitu vyenye ncha kali na hatari kwa kutumia njia ya majadiliano kwa vitendo.

    (b) Eleza faida tano (5) za kutumia zana halisi katika ufundishaji wa Vitendo vya Kujifunza Sayansi.

15. (a) Fafanua maana ya dhana ya utafiti wa kielimu na umuhimu wake katika uboreshaji wa mtaala.

    (b) Tofautisha malengo ya somo na malengo ya jumla katika somo la Vitendo vya Kujifunza Sayansi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

16. (a) Jadili hatua tano (5) za njia ya kisayansi unazopaswa kumfundisha mtoto wa elimu ya awali.

(b) Bainisha nyanja nne (4) za kiutendaji ambazo mwalimu anapaswa kuzipima katika somo hili.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org